


**WAKALA WA MAENDELEO YA UONGOZI WA ELIMU
(ADEM) - BAGAMOYO**



SHERIA ZA ADEM KWA WANACHUO

**ADEM
OCTOBER, 2017**

**WAKALA WA MAENDELEO YA UONGOZI WA ELIMU
(ADEM) - BAGAMOYO**



SHERIA ZA ADEM

1. Mwanachuo anatakiwa kuhudhuria masomo yote wakati wote akiwa chuoni isipokuwa tu kwa sababu maalum kama vile ugonjwa.
2. Ni marufuku kwa mwanachuo kujiamulia kuondoka ADEM kwa muda mfupi au mrefu pasipo rufusa ya Mshauri wa Wanachuo (Dean of students).
3. Mwanachuo anapaswa kutii sheria za nchi pamoja na taratibu zilizowekwa na ADEM .
4. Kila mwanachuo wa ADEM anapaswa kufahamu na kufuata kanuni, tabia na mwenendo mwema wa Mwalimu (Code of Professional Conduct).
5. Kila mwanachuo ajiheshimu mwenyewe kwa kuvaa mavazi yaliyo safi na ya heshima na kuwa na lugha yenye kutunza hadhi ya Meneja au Mthibiti Ubora wa Shule.
6. Kila mwanachuo anapaswa kuwaheshimu wenzake, wafanyakazi wa ADEM na watu wengine Katika jamii, nje na ndani ya Wakala
7. Ni kosa kwa mwanachuo kujiingiza katika tabia za uasherati au uzinzi na mtu yeyote. Ni kosa kwa mwanachuo kuonyesha kwa njia yoyote ile kwamba wanaishi kama wapenzi au wanandoa katika mazingira ya ADEM.
8. Mwanachuo hapaswi kuwa mlevi wa pombe, bangi au madawa ya kulevya ndani na nje ya Chuo.
9. Si rufusa kwa mwanachuo yeyote kwenda nyumbani kwa mfanyakazi wa ADEM bila kibali maalum.

10. Mwanachuo yeyote wa ADEM anapaswa kuvaa kitambulisho cha mwanafunzi alichopewa na ADEM muda wote awapo katika mazingira ya ADEM.

11. Mwanachuo anayeishi hosteli ya ADEM hapaswi kuwepo nje ya eneo la hosteli zaidi ya saa 6.00 usiku, mwanachuo anayeishi nje ya hosteli hapaswi kuwepo eneo la hosteli za ADEM baada ya saa 6.00 usiku.



Alphonse J. Amuli

K.n.y MTENDAJI MKUU

9 Oktoba, 2017

*For: Chief Executive
Agency for the Development of
Educational Management*